

TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA ISHIRINI NA TANO

Rejea taarifa iliyochapishwa kwenye vyombo vya habari kuhusu kuahirishwa kwa Mkutano Mkuu uliopangwa kufanyika tarehe 16 Mei, 2020.

TAARIFA inatolewa kwamba MKUTANO MKUU WA ISHIRINI NA TANO wa Wanahisa wa CRDB BANK PLC utafanyika siku ya Jumamosi, tarehe 27 Juni, 2020 kuanzia saa tatu kamili asubuhi na wanahisa watashiriki kwa njia ya kidijitali.

Benki itafanya Mkutano Mkuu mwaka huu kwa njia ya kidijitali ili kuepuka uwezekano wa maambukizi ya ugonjwa wa Corona kutokana na idadi kubwa ya wanahisa wanaotegemewa kuhudhuria Mkutano Mkuu na kutokuwepo Ukumbi wenye nafasi ya kutosha kwa washiriki wote wakiwa wamekaa na kutimiza taratibu na masharti yanayowataka watu kutokukaribiana na kupeana nafasi ili kujikinga dhidi ya maambukizi. Benki inachukulia kwa umuhimu wa kipekee afya na usalama wa wanahisa na wadau wake wote. Kwa kuwa na dhama na wajibu kwa jamii, Benki inaunga mkono juhudi za Serikali kupambana na ugonjwa wa Corona kwa kuzingatia taratibu zote za kiafya zinazotakiwa kufuatwa kama vile kuepuka mikusanyiko na kuzingatia watu kutokusongamana kwa kuachiana nafasi.

Benki itawatumia wanahisa wote kupitia simu zao za mkononi utambulisho na maelekezo kuhusu jinsi ya kujiunga na kushiriki Mkutano Mkuu kidijitali. Azimio maalum litapishwa na wanahisa ili kuruhusu Mkutano Mkuu ufanyike kwa njia ya kidijitali.

Dondoo zifuatazo zitajadiliwa :

1. Kufungua Mkutano.
2. Kuchagua Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Mkutano Mkuu.
3. Azimio Maalum kuidhinisha marekebisho kwenye Katiba ya Benki (MEMARTS) kuruhusu Mkutano Mkuu kufanyika kidijitali.
4. Kuridhia dondoo.
5. Kumtambulisha kwa wanahisa Mjumbe wa Bodi anayewakilisha Mfuko wa Uwekezaji wa DANIDA (DIF).
6. Kuthibitisha kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa Ishirini na Nne.
7. Kujadili yatakanayo.
8. Kupokea Taarifa ya Bodi ya Wakurugenzi na Taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa za Mwaka 2019.
 - a) Taarifa ya Bodi ya Wakurugenzi.
 - b) Hesabu zilizokaguliwa kwa Mwaka ulioishia tarehe 31 Disemba, 2019.
 - c) Azimio la Gawio kwa Mwaka 2019.

9. Kuidhinisha ada ya Wakurugenzi.
10. Kuteua Wakaguzi wa nje wa Hesabu.
11. Kuchagua wajumbe wawili Huru wa Bodi.
12. Kujadili mapendekezo kutoka kwa Wanahisa.
13. Mengineyo kwa idhini ya Mwenyekiti.
14. Kupanga mahali, ukumbi na tarehe ya Mkutano Mkuu ujao.
15. Kufunga Mkutano.

MAELEZO:

1. Daftari la Wanahisa litafungwa tarehe 26/06/2020 na litafunguliwa tarehe 27/06/2020.
2. Mapendekezo yote kutoka kwa wanahisa yatakayojadiliwa katika dondoo namba 12 yatumwe na kumfikia Katibu kabla ya saa 10.00 jioni siku ya Ijumaa tarehe 12 Juni, 2020.
3. Taarifa ya Mwaka 2019 na Makabrasha ya Mkutano yatapatikana kwenye tovuti ya Benki (<https://www.crddbbank.co.tz>) na matawi ya Benki kuanzia siku ya Ijumaa tarehe 12, Juni, 2020.
4. Wanahisa wanaombwa kuteua wawakilishi watakaohudhuria mkutano kwa njia yao. Fomu ya Uwakilishi inapatikana kwenye tovuti ya Benki (<https://www.crddbbank.co.tz>).
5. Fomu za Uwakilishi zilizojazwa zitumwe kwa Katibu kupitia barua pepe shareholders@crddbbank.com au zipeleke kwenye tawi lolote la Benki ya CRDB, au picha ya fomu ya uwakilishi iliyojazwa itumwe kwenye WhatsApp na.0767757215 na kumfikia Katibu kabla ya saa 10.00 jioni siku ya Jumatatu tarehe 22 Juni, 2020.

Kwa mawasiliano tumia anuani ifuatayo:

Katibu
CRDB Bank Plc
Office Accommodation Scheme- Azikiwe
Street, 4th Floor
S.L.P. 268
DAR-ES-SALAAM.
Simu. na. 022 - 2114237, 2117442 - 7
Barua Pepe - shareholders@crddbbank.com

KWA IDHINI YA BODI



J. B. Rugambo
KATIBU

20 Mei, 2020